



LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Kijitonyama, P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA

Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037, E-mail: lhrc@humanrights.or.tz

Website www.humanrights.or.tz

Tamko Kulaani Ukiukwaji wa Haki za Binadamu unaofanywa na Jeshi la Polisi

Kituo cha Sheria na Haki za binadamu kimesikitishwa na kitendo cha Jeshi la Polisi kuendeleza uvunjifu wa haki za binadamu na matukio ya kikatili dhidi ya wananchi kinyume na taratibu, sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni hivi karibuni Kituo cha Sheria na haki za Binadamu tumeungana marafiki wa haki za binadamu nchini Tanzania kukemea uvunjifu wa haki za binadamu unaofanywa na vyombo vya dola hususani vitendo vya kutweza utu na ukatili dhidi ya watazania.

Hivi karibuni vitendo vya jeshi la polisi kuingilia uhuru wa wanahabari na hata wanasiasa hasa wa upinzani vimeendelea kushamiri bila jeshi la polisi kuwajibika. Kitendo cha jeshi la polisi kumpiga mwandishi wa habari wa Wapo Radio Bw.Silas Mbise ambaye tayari alikuwa chini ya ulinzi wa polisi siku ya tarehe 08 Agost, 2018 Uwanja wa Taifa Jijini Dar es salaam ni mfano wa matukio ya hivi karibuni.

Kitendo hicho cha kikatili kimefanywa bila kuzingatia misingi ya utu na haki za binadamu, ikumbukwe kwamba Bw. Silas Mbise alikamtwa na kuwekwa chini ya ulinzi akiwa akitimiza majukumu yake ya kiandishi eneo la Uwanja wa Taifa lakini polisi walionekana wakimpiga mtuhumiwa ili hali akiwa amelala kuonesha amekubali kwamba yupo chini ya ulinzi.

Kifungu cha 21 cha Sheria ya Mwenendo wa Mkosa ya Jinai kinakataza matumizi ya nguvu kwa polisi wakati wa kumkamata mtuhumiwa;

21.-(1) Afisa polisi au mtu mwingine hatatakiwa, wakati wa kumkamata mtu, kutumia nguvu zaidi au kuvunja utu wa mtu huyo zaidi ya ilivyo lazima kufanikisha ukamataji au kumzuia utorokaji wa mtu baada ya kukamatwa. (2) Bila kupunguza matumizi ya kifungu kidogo cha (1), afisa polisi hatatakiwa, wakati wa kumkamata mtu, kufanya kitendo kinachoweza kusababisha kifo kwa

Board of Directors:

Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member, Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member, Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member

mtu huyo, isipokuwa kama afisa polisi anaamini kwa sababu za msingi kwamba kufanya kitendo hicho ni muhimu katika kulinda maisha au kuzuia madhara makubwa kwa mtu mwingine.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinalaani matumizi ya nguvu iliyotumika kwani ni kitendo cha kikatili dhidi ya utu wa binadamu na utawala wa sheria. Katiba ya Jamhuri ya Muungano ibara ya 13(6) (e) inakata kwa mtu yoyote kufanyiwa kitendo cha kikatili.

“ni marufuku kwa mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha”.

Kitendo kilichofanywa na askari wa jeshi la polisi ni tishio dhidi ya uhai wa mtuhumiwa kwani, imeonekana askari wawili wakimpiga Bw. Mbise kwenye mbavu na kichwani akiwa amelala chini kwa kujisalimisha kwa polisi wakati wa kumkamata.

Sambamba na tukio hili, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kimeshuhudia matukio mengine kadha wa kadha ya wanasiasa hasa wa vyama vya upinzani wakinyanyaswa na jeshi la polisi wakati kampeni za uchaguzi mdogo zikiendelea katika maeneo mbalimbali. Hivi karibuni, Jeshi la Polisi huko wilayani Tarime mkoani Mara waliripotiwa kuwanyasa viongozi wa yama vya upinzani na wafuasi wake kwa kuwatawanya, kuwapiga na hata kuwashikilia bila sababu za msingi.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinalitaka Jeshi la Polisi kufuata taratibu na sheria ikiwa ni pamoja na kuwajibika kuwachukulia hatua za kisheria askari polisi waliohusika katika tukio hili maana matukio haya yamekuwa yakijirudua mara kwa mara bila kuona hatua stahiki ziki-chukuliwa.

Imetolewa Agosti 10, 2018, na

**Bi. Anna Henga (Wakili)
Mkurugenzi Mtendaji**

Kwa Jamii yenye Haki na Usawa

Board of Directors:

Prof. Geoffrey R.V. Mmari - Chairperson, Ms. Anna Aloys Henga (Adv.) Secretary, Ms. Emeline A. Mboya - Member,
Mr. Thaddeo W. Mashera - Member, Dr. James E.M. Jesse (Adv.) - Member, Ms. Rebecca Z. Gyumi - Member,
Ms. Anastazia Rugaba - Member, Ms. Sophia M. Komba - Member